**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**MKOA WA MARA**
**HALMASHAURI YA WILAYA RORYA**

**SHULE YA SEKONDARI MIKA,**
**S.L.P. 250,**
**TARIME - RORYA.**
**01/12/2023**

SIMU: 0756397205 -MKUU WA SHULE
0756178301 -M/MKUU WA SHULE

KUMB Na; MSS/ADF1/VOL.1/01
JINA LA MWANAFUNZI .........................................................................................
SHULE YA MSINGI ATOKAYO; ..........................................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MIKA ILIYOPO KATA YA BUKWE WILAYA YA RORYA MKOA WA MARA**

Mkuu wa shule anayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika Shule hii. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **08/01/2024**. Shule hii ni ya kutwa tu. Tafadhali ieleweke kwamba utapokelewa kwa matumaini kuwa utaendelea na masomo yako kuanzia kidato cha **kwanza** hadi kidato cha **Nne**. Hatutapenda kuona unakatisha masomo kwa sababu zisizo za msingi.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1.1. SARE ZA SHULE.**

a) **Wasichana**

i. Mashati mawili meupe mikono mifupi.
ii. Sketi mbili (moja rangi nyeusi na nyingine rangi ya kaki). Ziwe na marinda yasiyopungua au kuzidi upana wa nchi tatu na ziwe ndefu **zinazovuka magoti nchi 14 na kuendelea kwenda chini.**
iii. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili.
iv. Tai yenye rangi sawa na sketi.
v. Viatu vya ngozi nyeusi tupu (bila mabaka) vya kufunga na kamba na visivyo na kisigino kirefu.
vi. Blauzi nyeupe za kuvaa ndani ya shati.
vii. Sweta moja rangi ya kaki yenye alama ya V shingoni. Nembo ya shule yenye maboresho itawekwaa shuleni (Usigonge nembo nje ya shule).
viii. T-Shirts ya kola ya rangi ya dark blue (nembo inapatikana shuleni)

ix. Track suit rangi ya bluu **isiyobana**.
x. Hijabu nyeupe kwa Wanafunzi wa Kike wa Kiislamu.

b) **Wavulana**

i. Mashati mawili meupe mikono mifupi.
ii. Suruali mbili (moja rangi nyeusi na nyingine rangi ya kaki). Ziwe na marinda mawili, **upana miguuni isipungue nchi 16.**

***NB: ZINGATIA suruali zilizobanwa chini haziruhusiwi kabisa.***

iii. Soksi nyeusi ndefu jozi mbili.
iv. Tai yenye rangi sawa na suruali.
v. Viatu vya ngozi nyeusi tupu (bila mabaka) vya kufunga na kamba.
vi. Fulana nyeupe za kuvaa ndani ya shati.
vii. Sweta moja rangi ya kaki yenye alama ya **V** shingoni. Nembo ya shule yenye maboresho itawekwaa shuleni (Usigonge nembo nje ya shule).
viii. T-Shirts ya kola ya rangi ya dark blue isiyo na nembo (nembo itagongwa shuleni).
ix. Track suit rangi ya bluu **isiyobana.**

**1.2. VIFAA VINGINE KWA WOTE.**

i. Picha za passport size nakala 2.
ii. Daftari zisizopungua 12 Counter Book.
iii. Lazima aje na mkebe wa vifaa vya hesabu (Mathematical set) na rula.
iv. Flat spring file ni lazima kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.
v. Dictionary ya English to English (***Mali ya mwanafunzi husika***).
vi. Begi jeusi la mgongoni la kubeba daftari.
vii. NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA.

**1.3. VIFAA VYA MICHEZO KWA WOTE.**

Mwanafunzi aje na viatu vya michezo (Kwa maana michezo ni ajira tusaidiane kuibua vipaji vya watoto wetu) .
***NB. Vifaa vyote vitakaguliwa.***

**1.4. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

i. Ni lazima kuwaheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii nzima kwa ujumla.
ii. Ni lazima kuhudhuria vipindi vyote vya darasani na katika shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Ni lazima kufika shule (saa moja kamili) na kushiriki shughuli zote za usafi.
iv. Ni lazima kufahamu mipaka yote ya shule.
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira muda wote uwapo shuleni.
vi. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
vii. Kutunza mali zako, za wenzio na mali za umma.
viii. Kuvaa sare ya shule wakati wote.

**1.5. MAMBO USIYORUHUSIWA KUFANYA UKIWA KAMA MWANAFUNZI.**

i. Kutembelea maeneo yoyote ya starehe, vilabu vya pombe, nyumba za kulala wageni.
ii. Kufuga nywele, kusuka na kunyoa nywele katika mtindo wowote mfano pank, kiduku n.k
iii. Kufuga kucha, kupaka rangi kucha na kutumia vipodozi vya aina yoyote ile, poda, makeup n.k
iv. Kuvaa mapambo ya aina yoyote ile mfano pete, mikufu, bangili za aina yoyote, heleni n.k.
v. Kutembelea nyumba za walimu bila kibali maalumu.
vi. Kutoka nje ya eneo la shule kwa muda wote unaopaswa kuwa shuleni bila kibali maalumu.
vii. Utoro wa rejareja.
viii. Kumiliki simu ya mkononi

**1.6. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Uasherati, ubakaji na ushoga.
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
iv. Uvutaji bangi.
v. Makosa ya jinai.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kupiga au kupigana.
viii. Kudharau bendera ya Taifa.
ix. Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
x. Kuoa au kuolewa.
xi. Kutoa mimba.
xii. Kugoma, kuchochea na kuongoza na ua kushiriki kuvuruga amani na usalama wa watu.

xiii. Kukataa adhabu kwa makusudi.
xiv. Kukutwa na simu ya mkononi.

**1.7. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI.**

i. **Medical examination form** (fomu ya hospitali) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali au kituo cha afya cha serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
ii. Fomu ya maelekezo binafsi ya mwanafunzi na mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule.
iii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iv. Mzazi au mlezi ni lazima umpatie mwanao chakula awapo shuleni.
v. Mwanao aje na meza na kiti ili akalie darasani.

**Karibu sana shule ya sekondari Mika.**

______________

**RAMADHANI SALEHE MWINYIKONDO**
**MKUU WA SHULE.**

**KIAMBATANISHO-A**

SHULE YA SEKONDARI MIKA,
S.L.P 250,
TARIME - RORYA.

**FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI**

JINA LA MWANAFUNZI; ……………………………………………………………..

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

a) Eye-sight……………………………….…………………….......................

b) Hearing………………………………….……………………………………….

c) Limbs…………………………………….……………………………………

d) Spleen………………………………………………………………………………

e) Venereal diseases ……………………………………………………………….

f) Leprosy …………………………………………………………………………….

g) Epilepsy…………………………………………………………………………….

h) Physical abnormality………………………………..………………………….

i) HB…………………………………………………………………………………

j) Pregnancy ………………………………………………………………………

k) Allergies……………………………………………………………………………

l) Other serious diseases ……………………………………….………………

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu ataweza/hawezi kuendelea na masomo ya sekondari.…………………… …………………………… …………………..

JINA LA HOSPITALI; ………………….............……….

JINA LA DAKTARI; ………………………………………

CHEO; ………………………………………………….….

SAHIHI; ……………………………….…………….. 

MUHURI NA TAREHE; ………………………………….

**KIAMBATANISHO- B**

**i. AHADI YA MWANAFUNZI (IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE).**

Mimi (Jina) ………………………………………………………niliyechaguliwa kidato cha kwanza shule ya sekondari Mika. Baada ya kusoma kwa makini sheria na kanuni muhimu za shule, naahidi kuzifuata. Nimekubali kwa hiari yangu kujiunga na shule ya sekondari Katuru. Endapo nitaenda kinyume na maelekezo hayo hatua za kisheria zichukuliwe.
Tarehe; ………………………………….. Sahihi; ……………………………………

**ii. MAELEZO YA MZAZI (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI).**

Mimi (Jina) ……………………………………………..mzazi/mlezi wa ……………… ……………………………… nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote na nimekubali mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari Mika. Endapo mtoto atakiuka maelezo hayo, hatua za kinidhamu zichukuliwe.
Tarehe; ………………………………….. Sahihi; ………………………………….